Toleo la 29

# jarida la WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Jarida la Mtandaoni | www.michezo.go.tz | Julai 05, 2022



# Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

# TAHARIRI

## HONGERA SERIKALI KUTUMIA KISWAHILI KWENYE MASUALA YA SHERIA



Mhariri
**JOHN MAPEPELE**

Serikali inaendelea na kazi ya kupitia sheria zote ili ziandikwe kwa lugha ya kiswahili ili watu wengi waweze kuzisoma na kuzielewa.

Waziri wa Sheria na Katiba, Dkt. Damasi Ndumbaro amefafanua suala hili jana mara baada ya kupokea maandamano ya kuelekea kwenye kilele cha siku ya Kiswahili duniani jijini Dar es Salaam.

Ameeleza kuwa dhamira ya Serikali kwa sasa ni kuhakikisha kuwa sheria zote zinaandikwa kwa kiswahili ambapo hadi sasa tayari zaidi ya nusu zimeshatafusiriwa kwa lugha ya Kiswahili.

Tunapongeza juhudi hizi za Serikali za kutumia kiswahili katika maeneo muhimu hususani sheria ili haki za wananchi ziweze kupatikana.


**BODI YA WAHARIRI**

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo
**Dkt. Hassan Abbasi**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo
**Saidi Yakubu**

Mhariri
**John Mapepele**

Waandishi
**Eleuteri Mangi**
**Shamimu Nyaki**
**Eliphace Marwa**

Wapiga Picha
**Joseph Kigingi**
**Projestus Binamungu**
**Abubakar W Kafumba**

Msanifu
**Abubakar W Kafumba**



# Rais Samia Atoa Vifaa vya Michezo kwa Timu Zote za Kombe la Yamleyamle

Na John Mapepele - **WUSM, Dar es Salaam**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Samia Suluhu Hassan ametoa vifaa vya michezo kwa timu zote 45 zinazoshiriki mashindano ya kombe la Yamleyamle Zanzibar ili timu ziweze kufanya vizuri hatimaye kuwapata wachezaji bora na wenye vipaji ambao wataunganishwa kwenye timu ya Taifa.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mhe. Mohamed Mchengerwa, Julai 3, 2022 wakati akizindua mashindano hayo yanayofanyika kwenye Uwanja wa Amani Zanzibar ambapo amesema Mhe. Rais ametoa mipira 45 kwa ajili ya timu hizo na jezi.

“Niwaombe tunapojipanga kwenda kuandaa mashindano ya AFCON, tuleteeni orodha ya vijana wanaofanya vizuri tutahakikisha tunawaingiza kwenye time zetu za taifa, tutawaendeleza, tutakuza vipaji vyao kwa maslahi ya Serikali zote mbili SMT na SMZ”. Amesisitiza Mhe. Mchengerwa. Amewapongeza kwa kuandaa mashindano hayo ambapo amefafanua kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kuwa inaandaa mashindano ya AFCON 2027 na kusisitiza kuwa inawezekana iwapo kila mdau atachukua wajibu wake.

Aidha, amefafanua kuwa eneo la soka ndilo eneo pekee ambalo linaweza kuwaunganisha watanzania wote bila kujali itikadi ya dini zao, rangi wala makabila yao.




# Naibu Spika Mhe. Zungu Aipongeza Wizara Kuandaa Tamasha la Usiku wa Taarabu

Na Eleuteri Mangi - **WUSM, Dar es Salaam**

Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mussa Azan Zungu amesema Tamasha la Usiku wa Taarabu ni fursa ya watu kupata burudani ambayo imeandaliwa vizuri na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Naibu Spika Zungu amesema hayo Julai 3, 2022 katika fukwe za Coco Beach zilizopo jijini Dar es Salaam ambapo hafla hiyo ilifanyika kwa usimamizi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

"Nampongeza Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, toka amemteua Waziri Mchengerwa na viongozi wanaoiongoza Wizara hii, mambo yamebadilika, kila kukicha tunasoma, tunaona na kusikiliza kwenye vyombo vya habari mambo mbalimbali mazuri yanayofanywa na wizara hii" amesema Naibu Spika Zungu.

Hafla hiyo imehudhuriwa na Naibu Waziri Mhe. Pauline Gekul, Katibu Mkuu Dkt. Hassan Abbasi, Naibu Katibu Mkuu Bw. Saidi Yakubu, Katibu Mwenezi wa CCM Taifa Shaka Hamidu Shaka, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni ambaye pia alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amos Makalla, watumishi wa wizara hiyo pamoja na wananchi ambao ni wapenzi wa muziki wa taarabu.



# Kiswahili Kinafanya Mahakama Kutembea 'Kifua Mbele'

Na Shamimu Nyaki - **WUSM, Dar es Salaam**

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro amesema mwelekeo wa Serikali katika kukiendeleza Kiswahili unafanya Mahakama kutembea 'kifua mbele' kwa kuzingatia usemi wa "Thamini chako".

Mhe. Ndumbaro amesema hayo Julai 4, 2022 Uwanja wa Uhuru jijini Dar es salaam wakati anapokea maandamano ambayo yanahusu Kiswahili na haki kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Utamaduni Duniani (MASIKIDU).

"Kiswahili chetu tu, ndicho tunachopaswa kujivunia kila siku, lugha za wengine siyo zetu. Kwa hiyo, Kiswahili ndiyo lugha pekee ambayo imetufanya Watanzania kwa miaka sitini ya uhuru, kuishi pamoja na kufanya shughuli zetu kwa undugu, utulivu, amani na umoja.

Hatua hiyo imekifanya Kiswahili kupigiwa upatu kitumike katika masuala yote ya kisheria ikiwa ni pamoja na kanuni zake zote ambapo Mahakama ya Tanzania ikiwa mdau wa Kiswahili wanaamini uamuzi unaofanywa na serikali ni wa kizalendo na utawawezesha Watanzania na wananchi kupata fursa za kushiriki katika shughuli za ukalimani, tafsiri, uhariri, uandishi na uchapishaji wa vitabu vya sheria kwa Kiswahili.

Hizi ni jitihada za kuwawezesha wananchi kupata haki zao za kuelewa kinachoamriwa na kuandikwa katika michakato ya uendeshaji wa mashauri kuanzia ngazi za mabaraza ya

usuluhishi hadi mahakama za juu.

Mhe. Dkt. Ndumbaro ameigiza Wizara ya Katiba na Sheria kushirikiana na Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) kuendelea kutafsiri Sheria na Kanuni zote kwa Kiswahili ili wananchi wawawe na nafasi ya kupata uelewa wa mwenendo wa kesi zao na hatua inayosaidia kupata haki zaoT bila kumwonea mtu.

Aidha, Waziri Dkt. Ndumbaro amesema kuwa Mahakama za Tanzania utaratibu wa kuwa Mahakama za kimtandao na kutafuta programu ya akili bandia ambao ni mfumo wa kutafsiri na kuandika taarifa za mashauri mahakamani kwenye lugha zaidi ya kumi ikiwamo lugha ya Kiswahili.

Zaidi ya hayo, amesema Programu hiyo itakuwa na hatimiliki ya modeli ya Kiswahili na itakuwa chini ya Mahakama ya anzania ili Mahakama zingine duniani zikitaka kutumia, lazima wapate kibali cha Mahakama ya Tanzania na walipe tozo ya leseni ambayo ni chanzo cha mapato kwa Serikali.

Naye Katibu Mtendaji wa BAKITA Consolata Mushi amesema kuwa Tanzania ndiyo asili ya Kiswahili ambapo Kiswahili kinatumika kutoka kunakucha hadi kunakuchwa, watu wanaitumia lugha hiyo katika kutekeleza majukumu yao kitaifa, kiuchumi, kijamii na kisiasa.





# Shamrashamra kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani yapamba Moto

Na John Mapepele - **WUSM, Dar es Salaam**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Saidi Yakubu amesema Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani yameanzia Julai 04, 2022 kwa Matembezi ya hiari ikiwa ni kuunga mkono matumizi ya lugha hiyo katika haki.

Amesema hayo alipotoa neno la utangulizi na kumkaribisha Mgeni Rasmi, Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Damas Ndumbaro kuzungumza na hadhira iliyokuepo katika Uwanja cha Uhuru Jijini.

Bw.Yakubu amesema katika kuelekea Kilele cha lugha hiyo kutakua na shughuli mbalimbali ikiwemo Mdahalo wa Mchango wa Lugha ya Kiswahili katika Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika pamoja na Midahalo ya wanamajumui wa lugha hiyo.

Aidha, amesema Siku ya Kilele ambayo ni Jalai 07, 2022 Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Philipo Isdor Mpango hafla itakayofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.




# Kiswahili Chazidi Kuitangaza Tanzania Kimataifa

Na Shamimu Nyaki - **WUSM, Dar es Salaam**

Kiswahili imechangia kuitangaza Tanzania kutokana na lugha hiyo kuwa miongoni mwa lugha zenye wazungumzaji wengi ulimwenguni.

Akizungumza katika siku ya Maandamano ya hiari ya kuelekea Siku ya Kiswahili Duniani, Julai 03, 2022 Dar es Salaam Katibu Mtendaji wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) Bi. Consolata Mushi amesema lugha hiyo imepata heshima kubwa kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuitengea siku yake maalum ya kuadhimishwa ambayo ni Julai 07 ya kila Mwaka.

"Maadhimisho haya ni kudumisha heshima tuliyopewa na UNESCO kama watumiaji wa lugha hiyo, na tutaitumia fursa hii kukuza na kuendeleza lugha yetu adhimu kwa vizazi vyote" Amesema Bibi. Consolata.

Ameongeza kuwa, hivi karibuni lugha hiyo ilipitishwa kuwa lugha ya kazi ndani ya Umoja wa Afrika lakini pia imepewa heshima pia kuwa lugha ya Mawasiliano ndani ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Aidha, ameipongeza Wizara ya Katiba na Sheria kwa jitihada za kuhakikisha lugha hiyo inatumika katika Mahakama, lakini pia kuendelea kuchukua hatua za kutafsiri Sheria ziwe katika Lugha ya Kiswahili.

Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili kitakua Julai 07, 2022 Dar es Salaam.



# Wimbo wa "Dunia Siyo Mali yetu" Wakonga Mashabiki wa Taarabu Usiku wa Taarabu

Na Eleuteri Mangi - **WUSM, Dar es Salaam**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Maji na Madini kutoka nchini Burundi ndugu Seleman Khamissi amesema nchi hiyo ni ndugu na Tanzania wakati wote wa raha na shida.

Katibu Mkuu huyo amesema hayo wakati wa Tamasha la Usiku wa Taarabu lililofanyika Julai 3, 2022 katika fukwe za Coco Beach zilizopo jijini Dar es Salaam ambapo vikundi mbalimbali vya taarabu kutoka ndani nan je ya nchi walipata fursa ya kutumbuiza mashabiki wa muziki huo.

"Nashukuru sana kwa mwaliko huu, kwetu sisi Tanzania ni mzazi, tukiwa na shida na raha tupo pamoja. Asanteni sana kwa kushirikiana nasi Burundi" amesema Katibu Mkuu ndugu Seleman.

Katika tamasha hilo, Kikundi cha Al Watan Taarabu ambapo awali kilijulikana kama "Super Star" cha nchini Burundi kimekuwa kivutio kwa wimbo wao unaojulikana kwa jina la "Dunia siyo mali yetu" ambao mahadhi yake yamejaa mafundisho kwa kuwakumbusha wanadamu kuwa wasijivune na ukadharau wakidhani watadumu.

Aidha, Katibu Mkuu huyo ametoa zawadi ya ngoma ya asili kutoka Burundi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan na kwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Mohamed Mchengerwa ikiwa ni ishara ya kuthamini Utamaduni baina ya nchi hizo mbili. Ngoma hiyo inatambuliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kama urithi wa Utamaduni wa nchi hiyo.

Taarabu ni aina ya muziki ya Afrika ya Mashariki wenye asili yake katika utamaduni wa Waswahili ambao hupendwa sana na wakazi wa miji ya pwani ya Bahari Hindi katika Afrika ya Mashariki, hasa Tanzania na Kenya, ambao ni wasemaji asili wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kwanza.

# WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano
Serikalini - GCU

**Mawasiliano**
P.O. Box 25, Dodoma,Tanzania
Mji wa Serikali Mtumba
Telephone: +255 26 2322 129
Nukushi: +255 26 2322 128
Barua pepe: km@habari.go.tz